**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**
**SHULE YA SEKONDARI UBIRI**

**Namba za Simu-0757127862**
**Mkuu wa ShuleJENIPHER H LAURICH Makamu Mkuu wa Shule.KHALIFAN A VUAI - 0625866350**
**Matron/Patron.MWANAIDI A RAJABU - 0628946325**
**Shule ya Sekondari UBIRI S.L.P.308- LUSHOTO Tarehe ……………**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**…………………………………………**
**….. S.L.P**
**………………………………………..**
**………………………………………………**

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI UBIRI HALMASHAURI YA LUSHOTO MKOA WA TANGA MWAKA …………………………….**

**SEHEMU A: UTANGULIZI**

1. Hongera kwa kuchaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano mwaka ………….katika shule ya Sekondari Ubiri, Tahasusi ya **HKL, HGL,HGLi, HGFa na HGK**
2. Shule ya sekondari Ubiri ipo Lushoto mjini katika mkoa wa Tanga. Ukitokea Mombo shuka kituo kinachoitwa **MALWATI** kabla ya kufika Lushoto mjini**.** Vivyo hivyo kutoka Lushoto mjini utapanda magari yanayoelekea Soni – Mombo na kushuka kituo kinachoitwa **MALWATI** na hapo utaona kibao kinachoelekeza shule ilipo. Kutoka maluati kwenda shule ilipo utachukua usafiri wa pikipiki ambao gharama yake haizidi shilingi elfu mbili (2000)
3. Ukiwa Ubiri Sekondari, utalazimika kufuata Sheria, Kanuni, Taratibu za Shule (kamilisha kiambatanisho A na B ).

**SEHEMU B: SARE YA SHULE NA MAHITAJI MENGINE**

| NA. | SARE/MAHITAJI | MAELEZO |
|---|---|---|
| 1 | Mashati 2 meupe ya Mikono mirefu,Tetroni (Lisiwe linalo bana au linalo onesha ndani) | Anunue duka lolote |
| 2 | Sketi 2 ndefu zinazofika kwenye kifundo cha mguu (ankle) iwe ''rinda box''katikati na marinda matatu kila upande yaani kulia na kushoto ya rangi ya karoti. | Anunue duka lolote |
| 3 | Masweta 2 ya rangi ya Bluu iliyokolea ( dark blue) ya 'V' (yasiwe ya vifungo) au zaidi yenye nembo ya shule. | Yanapatikana shuleni kwa bei ya Tsh 15,000/= kila moja kwa anae hitaji. |
| 4 | Viatu vyeusi vya ngozi jozi 2 vya kufunga na kamba(visiwe vyenye visigino virefu), na soksi nyeupe. | Anunue duka lolote |
| 5 | Tai mbili za kipepeo za rangi ya karoti(rangi ya sketi) kwa wale wasiovaa Hijab,<br>Na pull neck nyeusi kwa ajili ya baridi | Anunue duka lolote |
| 6 | T-shirt 2 za shule @ Tsh. 15,000/= zenye nembo ya shule. | Fika na fedha taslim ya kununulia (zinapatikana shuleni kwa anae hitaji. |
| 7 | Shuka 2 za rangi ya pink | Anunue duka lolote |
| 8 | Blanketi, au mashuka mazito ya kujifunika, pamoja na chandarua | Anunue duka lolote |
| 9 | Godoro imara la ukubwa wa futi mbili na nusu kwa sita.(Godoro Dodoma au Comfy) | Yanapatikana shuleni kwa bei ya tsh 55,000/= kwa anae hitaji. |
| 10 | Picha nne passport size | Apige popote |
| 11 | Magauni mawili (2) ya rangi ya kijivu (Grey) iliyokolea, ya mshono wa solo na marefu mpaka kwenye kifundo cha mguu.shingo ya round na mikono mifupi kwa wakristo na mikono mirefu kwa waislam pia hijabu inayofanana na gauni. | Anunue duka lolote |
| 12 | Kwa wanafunzi wa kiislamu watakaopenda kuvaa Hijabu wataruhusiwa kuvaa sketi ndefu za karoti, mashati meupe (nusu kanzu), sweta la dark blue na Hijabu nyeupe tu isiyo na urembo. | Anunue duka lolote |
| 13 | Sanduku imara la bati (tranker) kwa ajili ya kuhifadhia vifaa vyako | Anunue duka lolote |
| 14 | Track suit ya rangi ya bluu ya mawingu (light blue) yenye nembo ya shule. | Zinapatikana shuleni kwa bei ya Tsh 30,000/= kwa anae hitaji. |
| 15 | Raba nyeupe kwa ajili ya michezo | Anunue duka lolote |
| 16 | Vifaa vya chakula ikiwa ni pamoja na Kijiko ,sahani, kikombe na bakuli | Anunue duka lolote ila visiwe vya plastiki |
| 17 | Ndoo ndogo moja na kubwa moja | Anunue duka lolote |

**SEHEMU C: VIFAA VYA USAFI**

| S/N | VIFAA | TAHASUSI | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| 01 | Jembe, Hard broom fupi ya kusugulia sinki la chooni, Chelewa, na fyekeo | HKL | Anunue duka lolote |
| 02 | Mopper na dekio lake,ndoo na dekio lake la utambi | HGFa | Anunue duka lolote |
| 03 | Jembe, (squeezer) ufagio wa kukaushia maji chooni na bafuni, Chelewa, Na fyekeo | HGL | Anunue duka lolote |
| 04 | Jembe, Soft broom (mifagio ya kufagilia ndani, chelewa | HGLi | Anunue duka lolote |
| 05 | Jembe, fyekeo na chelewa | HGK | Anunue duka lolote |

**VIFAA VYA DARASANI**

1) Ufike na daftari kubwa counter book quire3 tisa(9) na daftari ndogo (normal) tisa kwa ajili ya mazoezi ya darasani kwa masomo 4 utakayo soma, kalamu na mkebe (Mathematical Set kwa watakaosoma somo la Jiografia) na Non programable calculator
2) Dictionary ya kiingereza kwa kiingereza 1, kamusi ya kiswahili kwa kiswahili 1na kiswahili kwa kiingereza 1 kwa matumizi binafsi na kwa masomo ya tafsiri na ukalimani kwa somo la Kiswahili na Kiingereza.
3) Karatasi kwa ajili ya mitihani Rimu 2 -A4 – Na Vitabu vya ziada.

**SEHEMU D: MICHANGO MINGINE**
**(LIPA KWENYE AKAUNTI YA NMB NAMBA 41603500079 YENYE JINA LA UBIRI SECONDARY SCHOOL)**

| NA | AINA YA MCHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Nembo | 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| **JUMLA** | | **80,000/=** |

**MUHIMU:**

1. Mwanafunzi aje na risiti ya malipo bank pay in slip (**BPS**)
2. Mwanafunzi atapokelewa tu iwapo amekamilisha kulipa michango mingine na kukabidhi vifaa vyote vilivyoagizwa.
3. Mwanafunzi anashauriwa kuwa awe na fedha za mfukoni (pocket money) kwaajili ya kujikimu.
4. Wanafunzi wote hawaruhusiwi kusuka/ ama kufuga nywele
5. Unaposafiri, **uvae sare ya shule na ufike shuleni ukiwa katika sare ya shule**
6. Ukifika shuleni ripoti moja kwa moja kwa Mkuu wa Shule kisha taratibu nyingine zitafuata.

7. Mwanafunzi aje na bima ya afya ya Taifa iliyokatwa na mzazi ya kiasi chTsh **50,400/=**

10. Mwanafunzi ataruhusiwa kutembelewa na mzazi/ mlezi au ndugu ambae taarifa zake zipo ofisi ya mkuu wa shule. Mzazi atajaza fomu na kubandika picha za ndugu watakao mtembelea.

**N/B:** Mzazi / mlezi au ndugu hataruhusiwa kumuona mwanafunzi tofauti na siku iliyoainishwa hapo juu**.**

Hakikisha unasoma kwa makini maelezo haya na kuyatekeleza kikamilifu Karibu sana Shule ya Sekondari Ubiri.

**JENIPHER HENRICH -MKUU WA SHULE 0757127862/0627274115**

**KIAMBATANISHO A**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO**
**SHULE YA SEKONDARI UBIRI**

FOMU YA TAARIFA ZA MWANAFUNZI

***A: AJAZE MWANAFUNZI***

1. JINA KAMILI..............................................................................................................................
2. TAREHE YA KUZALIWA....................................................................................
3. URAIA..........................................................
4. DINI.............................................................
5. SHULE ULIYOSOMA AWALI: -

SEKONDARI..........................................MWAKA WA
KUANZA......................KUMALIZA......................

**SAINI YA MWANAFUNZI: ................................. TAREHE...............................................**

**B: MAELEZO YA MZAZI/MLEZI (AJAZE MZAZI/MLEZI)**

1. JINA LA BABA................................................................... SAINI............................................
KAZI.....................................................................
ANWANI ......................................................................SIMU..............................................
2. JINA LA MAMA.............................................................SAINI..........................................
KAZI.................................................................................
ANWANI .....................................................SIMU.............................................................

**C: AHADI YA MZAZI:**

Mimi mzazi wa mwanafunzi ................................................................... naahidi kuwa nitashirikiana na uongozi wa shule na walimu kusimamia nidhamu ya mtoto wangu na kuhakikisha anasoma kwa bidii na kufaulu. Aidha natambua kuwa simu haziruhusiwai shuleni na hivyo naahidi kuwa sitampa simu na endapo atabainika kuwa na simu anastahili kufukuzwa shule kwa mujibu wa sheria za shule.

Mimi .....................................................................Mzazi/Mlezi wa..................................................
Saini....................................................... Tarehe.............................................

**KIAMBATANISHO B**

**PRIME MINISTER'S OFFICE: REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**LUSHOTO DISTRICT COUNCIL**

UBIRI SECONDARY SCHOOL

P. O BOX 308
**LUSHOTO**

Ref No. SSS/PS/V.1/12
To The Medical Officer
......................................
......................................

**REF: STUDENT'S MEDICAL EXAMINATION**

Please, examine the student named ..........................................................................................considering the areas mentioned below and any other area(s) applicable.
Does the student have problems with reference to the following?

a) Sight Yes/ No. If yes state.
.............................................................................................................................................................
...........................................................................................................................................
b) Hearing Yes/No. If yes state
.............................................................................................................................................................
...........................................................................................................................................
c) T.B or any other chronic diseases. Yes/No. If ye state.......................................................................................................................................................
...........................................................................................................................................
d) Blood Pressure. Yes/ No. If yes state
.............................................................................................................................................................
...........................................................................................................................................
e) Any physical impairment (s) Yes/ No. If yes state
.............................................................................................................................................................
...............................................................................................................................................

**DOCTOR'S RECOMMENDATIONS**

Do you recommend the student to pursue studies in this school?
..................................................................................................................................................

Doctor's Name .............................................Signature.............................. Date..........................

Official Title................................................. Official stamp

## KIAMBATANISHO C

### 1. HESHIMA

a) Mwanafunzi atasimama kumsalimia Mwalimu au mtu yoyote aliyemzidi umri anapopita,anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.
b) Mwanafunzi atatumia lugha safi(inayokubalika) wakati wowote kati yake na wenzake na kwa watu wengine akiwa shuleni au nje ya shule.
c) Mwanafunzi anatakiwa kuwaheshimu wafanyakazi wote walioko shuleni kama walezi wake.
d) Mwanafunzi ataitika wito maramoja na kukimbilia aliko Mkuu anayemwita.
e) Mwanafunzi anapaswa kuheshimu kazi yeyote anayopewa na Mwalimu au Mlezi na anatakiwa ashirikiane na wenzake ili kuifanya kazi hiyo.
f) Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu Bendera ya Taifa na picha za viongozi wa serikali,nembo ya Taifa,wimbo wa Taifa na fedha za Taifa.
g) Mwanafunzi atasimama katika mstari wakati wowote anaposubiri kupata huduma.
h) Mwanafunzi atakaa kimya wakati wowote akiwa darasani,asitoke nje ya darasa au eneo la shule bila ruhusa ya Mwalimu.Atatoka nje ya eneo la shule kwa siku zilizotangazwa au ruhusa.

### 2. MAHUDHURIO

a) Mwanafunzi anatakiwa ahudhurie vipindi vyote vya darasani kwa muda wote wa masomo. Atatakiwa kufika shuleni kwa tarehe zote zilizopangwa na anapokosa kufika siku anapofika akatoe taarifa kwa mmojawapo wa hawa:
   i. Mwalimu wa zamu siku hiyo.
   ii. Mwalimu wa darasa.
   iii. Makamu wa Mkuu wa Shule.
b) Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria mikutano yote ya shule kama vile Baraza la Shule,Ukaguzi wa usafi na Kupandisha Bendera ya Taifa.
c) Mwanafunzi atatakiwa kuwahi shughuli zote shuleni kama zilivyopangwa kwenye ratiba ya shule.Tena anatakiwa kuwahi anapotakiwa au anaposikia kengele.
d) Mwanafunzi anatakiwa kufanya mazoezi,majaribio na mitihani yote anayopewa na Mwalimu wa somo darasani.Akikosa jaribio au mtihani wowote,akamuone Mwalimu wa somo na Mwalimu Mwandamizi Taaluma.

### 3. SARE YA SHULE NA USAFI

Mwanafunzi anatakiwa kuwa katika sare safi ya shule wakati wote wa saa za shule. Atakuwa na vazi tofauti pale tu atakapoagizwa kama vile nguo za michezo wakati wa michezo.

**MAKATAZO:**

### 4. SEHEMU ASIZORUHUSIWA KUTEMBELEA MWANAFUNZI

a) Mwanafunzi asitembelee sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali au ruhusa:
   i. Ofisi ya Walimu
   ii. Maabara
   iii. Nyumba za Walimu na Wafanyakazi.
   iv. Chumba cha Walimu au Wafanyakazi

b) Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kutembelea sehemu hizi:

i. Vilabu vya pombe
ii. Nyumba za starehe
iii. Nyumba za kufika wageni

c) Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya eneo la shule bila ruhusa/kibali maalumu.

5. NI MARUFUKU:

a) Kuiba mali ya mtu binafsi a la umma.
b) Kufanya uasherati,ubakaji au ushoga.
c) Kulewa kilevi cha aina yeyote au kuvuta sigara au bangi.
d) Kupiga au kupigana.
e) Kuharibu mali ya umma.
f) Kuoa au kuolewa.
g) Mwanafunzi kumiliki/kuwa na simu shuleni.

6. MAKOSA YANAYOFUKUZISHA SHULE:

a) Uasherati,ubakaji na ushoga,kuoa au kuolewa.
b) Wizi,ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.
c) Kuvuta bangi.
d) Kupiga au kupigana.
e) Kudharau Bendera ya Taifa,kuharibu mali ya umma.
f) Kupata,kutoa mimba au kusababisha mimba shuleni au nje ya shule.
g) Kugoma,kuongoza,kuchochea mgomo au vurugu,kuchafua amani au usalama wa watu.
h) Kukashifu na kukataa adhabu halali.

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule :0757127862**
- **Makamu Mkuu wa Shule :0625866350**
- **Mwandamizi Taaluma: 0621659597**
- **Mwandamizi Malezi: 0628946325**

……………………

**JENIPHER H LAURICH.**
**MKUU WA SHUL**

**KIAMBATANISHO D**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO**
**SHULE YA SEKONDARI UBIRI**

FOMU YA TAARIFA ZA NDUGU WATAKAOMTEMBELEA MWANAFUNZI SHULENI

1) JINA KAMILI ................................................................
   TAREHE YA KUZALIWA ....................................................
   DINI....................................
   URAIA ......................
   UHUSIANO WAKE NA MWANAFUNZI ..........................................
   NAMBA YA SIMU ....................................................... SAINI.................

   PICHA

2) JINA KAMILI ................................................................
   TAREHE YA KUZALIWA ....................................................
   DINI....................................
   URAIA ......................
   UHUSIANO WAKE NA MWANAFUNZI ..........................................
   NAMBA YA SIMU ....................................................... SAINI.................

3) JINA KAMILI ................................................................
   TAREHE YA KUZALIWA ....................................................
   DINI....................................
   URAIA ......................
   UHUSIANO WAKE NA MWANAFUNZI ..........................................
   NAMBA YA SIMU ....................................................... SAINI.................

4) JINA KAMILI ................................................................
   TAREHE YA KUZALIWA ....................................................
   DINI....................................
   URAIA ......................
   UHUSIANO WAKE NA MWANAFUNZI ..........................................
   NAMBA YA SIMU ....................................................... SAINI.................

**Maelekezo muhimu:**

i. Muda wa kumtembelea mwanafunzi ni kuanzia saa mbili kamili asubuhi hadi saa tisa kamili mchana
ii. Mzazi/ ndugu hataruhusiwa kuingia na chakula shuleni.
iii. Mzazi/ ndugu ataruhusiwa kumtembelea mwanafunzi jumapili ya mwisho wa mwezi tu.
iv. Ndugu/ mzazi amabe taarifa zake hazipo shuleni hataruhusiwa kumtembelea mwanafunzi.